

# Simbachawene aitaka TAKUKURU kudhibiti rushwa fedha za miradi

Na **ESTA MALIBICHE**, Iringa

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, ameitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kudhibiti rushwa katika fedha za miradi ya maendeleo.

Alitoa kauli hiyo mkoani Iringa, alipotembelea na kukagua ujenzi wa jengo la ofisi za TAKUKURU, ambapo alimtaka mkandarasi kukamilisha ujenzi ifikapo Juni mwaka huu, kama ilivyopangwa ili watumishi waanze kazi katika mazingira rafiki.

"Tukawe watu wa kupekenyua kwenye miradi hii inayotekelezwa na serikali, kuna watu wanatumia vibaya fedha za serikali, penyeni kuwadhibiti ili miradi ya maendeleo ikamilike kwa wakati na viwango kama ilivyokusudiwa," alisisitiza.

Alisema TAKUKURU inatakiwa kusimamia na kudhibiti fedha zisipotee bila kuathiri maendeleo ya miradi ya kimkakati inayotekelezwa nchini.

"Palipo na shilingi ya Mama Samia



**Palipo na shilingi  
ya Mama Samia  
waambieni TAKUKURU  
tupo, lakini katika  
kufanya haya  
tusikwamishe  
maendeleo"**

George Simbachawene

waambieni TAKUKURU tupo, lakini katika kufanya haya tusikwamishe maendeleo," alisema Simbachawene.

Katika hatua nyingine, Waziri huyo aliitaka Taasisi hiyo kuwachukulia hatua wanaokwamisha shughuli za maendeleo.

"Dhibitini mianya ya kuchezea rasilimali za nchi ikiwemo fedha zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, sehemu ambako fedha imesimamiwa vizuri matokeo mazuri yameonekana," alisema Simbachawene.